

1. Sheria ya uvuvi haitakikani kulikimbiza kwa pamoja aina mbalimbali za uvuvi na mazuio yake. Kwa sababu ya tofauti za mfumo wa ikolojia na aina ya uvunaji rasilimali. Sheria ya uvuvi lazima itambue tofauti hizi.
2. Sisi hatuhusishwi na hatushirikishwi sana katika mipango na harakati za uundaji wa sera. Njia za kuwasilisha maoni na matatizo yetu ni chache na duni. Tunaomba wavuvi wajumuishwe vilivyo kwa uundaji wa sera kupitia mitandao ya wavuvi ya mashinani na ya kitaifa. "Kenya Marine Forum" inaweza pia kutuwakilisha.
3. Maeneo ya kinga ya ufuoni yamevamiwa na wastawishaji wa kibinafsi kutokana na unyonge wa kudhibiti sheria na ukosefu wa utiifu. Tunahitaji kuwa wakali mno juu ya udhibiti na utiifu wa sheria.
4. Hakuna nyaraka au hati ya utafiti inayothibitisha uwiano na uhusiano kati ya sheria bora, usimamizi endelevu wa uvuvi na manufaa ya kiuchumi na jamii. Hivi basi tunaona vigumu kupata motisha. Tugenda utafiti ufanywe kwa jambo hili ili tuone kinagaubaga uhusiano uliopo kati ya sheria na usimamizi bora wa uvuvi na kuboresha masilahi na uchumi wa jamii pamoja na upunguzaji wa umaskini.



